MATOKEO YA MSINGI

UTAFITI WA MAPATO NA MATUMIZI YA KAYA BINAFSI 2000/01

Dar es Salaam, Julai 2002

OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU
TANZANIA

Picha zilizotumiwa katika ripoti hii ni kwa fadhila ya
Adam Rogers, UNCDF

Kimepigwa chapa na Colour Print Tanzania Limited

UTAFITI MKUBWA WA MAPATO NA MATUMIZI YA KAYA BINAFSI ULIOWAHI KUFANYIKA TANZANIA BARA.

Ripoti hii inaonyesha (inatoa) vidokezo vya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi Tanzania Bara ya mwaka 2000/01 uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS). Ulikuwa utafiti mkubwa wa aina yake uliowahi kufanyika nchini Tanzania, ukihusisha zaidi ya kaya 22,000 – na ni mafanikio muhimu kwa NBS.

NBS ni wakala wa serikali wanaojitegemea. Madhumuni yake ni:

"… Kuwezesha utoaji maamuzi ndani ya serikali na katika jumuiya za kibiashara, kuchochea tafiti na mijadala kwa upatikanaji wa takwimu muhimu zinazoaminika na zinazopatikana kwa wakati na huduma za takwimu zenye ubora…"

Utafiti huu utakuwa msingi wa kufuatilia maendeleo yanayotokana na sera za serikali za kutokomeza umaskini. Halikadhalika, unaonyesha mwenendo wa vigezo vingi vya umaskini katika miaka ya 1990. Vipengele muhimu katika kurasa zifuatazo vimeelezwa kwa kina kwenye Ripoti kuu ya utafiti huu.

Utafiti utakuwa ni mchango muhimu katika kufuatilia na hatimaye kutokomeza umaskini nchini Tanzania. Ripoti hii ya matokeo ya msingi ni mwongozo muhimu unaoweza kumsaidia kila mtumiaji.

Mh. Dr. Abdallah O. Kigoda
Waziri wa Nchi
Ofisi ya Rais
Mipango na Ubinafsishaji

KUHUSU UTAFITI WA MAPATO NA MATUMIZI WA KAYA BINAFSI

Upimaji wa mwenendo katika umaskini.

Kutokomeza umaskini ni lengo kuu la sera ya Serikali ya Tanzania. Mipango kwa ajili ya kutokomeza umaskini iliainishwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Umaskini wa Juni 1998 na Mkakati wa Kupunguza Umaskini wa Oktoba 2000. Vyote vimesisitiza umuhimu wa ukuaji wa uchumi wa haki na endelevu na uboreshaji wa huduma za jamii za msingi.

Uchambuzi wa utafiti huu unalenga katika vigezo vya umaskini vilivyoainishwa katika mikakati hii. Unatoa taarifa kitaifa na kimkoa kuhusu vigezo hivi na msingi wa kutathmini maendeleo ya baadaye. Ikilinganishwa na utafiti kama huu wa 1991/92, utafiti wa hivi karibuni una mengi ya kusema kuhusu mwenendo wa vigezo vya umaskini katika miaka ya 1990 na matokeo ya sera zilizofuatwa katika kipindi hicho.

Ripoti hii fupi inadokeza matokeo ya msingi ya utafiti wa 2000/01. Haya yameelezwa kikamilifu kwenye ripoti kuu.

Zaidi ya Kaya 22,000 zilihojiwa.

Sampuli wakilishi kitaifa ya kaya 22,178 zilihojiwa – ikihusisha kati ya Kaya 12 na 24 katika kila eneo la sampuli lililochaguliwa na karibu kaya 1,000 katika kila mkoa wa Tanzania Bara. Utafiti kama huu wa mwaka 1991/92 ulikusanya taarifa zinazofanana sana na za mwaka 2000/01, ingawaje utafiti ulikuwa mdogo sana ukijumuisha kaya 4,823 tu.

Takwimu zilikusanywa kuhusiana na hali kwa ujumla ya mtu binafsi na kaya, zikijumuisha:

- elimu ya wanakaya, shughuli za kiuchumi na hali ya afya
- matumizi na mapato ya kaya
- umiliki wa vifaa vya kudumu na raslimali
- Hali ya nyumba na vifaa vya ujenzi, na
- upatikanaji wa huduma na mahitaji ya kaya.

Dodoso moja kuu pamoja na shajara ya kuweka kumbukumbu ya matumizi, gharama na mapato ya kaya kwa mwezi mmoja wa Kalenda vilitumika. Wanakaya walitumia shajara binafsi kuandika matumizi mbali na nyumbani.

Utafiti wa 2000/01 unatoa taarifa ya watu wa Tanzania Bara kwa ujumla na ya Dar es Salaam peke yake, maeneo mengine ya Mjini na ya Vijijini na kwa kila mkoa. Utafiti kama huu wa 1991/92 ulikuwa mdogo na haukuweza kutoa taarifa za kuaminika kimkoa.

MAPITIO YA UMASKINI NA USTAWI WA JAMII TANZANIA BARA.

Maendeleo mengi yametokea zaidi katika maeneo ya mjini. Yamekuwa madogo katika maeneo ya vijijini.

Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi 2000/01 wa Tanzania Bara unathibitisha kuwa umaskini wa kipato ni mkubwa na vigezo vya ustawi wa jamii kwa kawaida ni duni. Pia unaonyesha tofauti kubwa kati ya makundi mbalimabli. Tofauti kubwa zaidi ni kati ya watu wa mjini na wa kijijini. Kwa upande mmoja, Dar es Salaam ina unafuu zaidi kuliko sehemu nyingine ya nchi; na kwa upande mwingine, kaya za vijijini ni maskini zaidi kuliko kaya kama hizo za mjini karibu katika mambo yote. Haja ya kulenga katika kuondoa umaskini maeneo ya vijijini inabakia kuwa jambo la lazima. Kimkoa, tofauti za vigezo hivyo zinaonekana kuwa kubwa sana. Hata hivyo, inawezekana kuitambua mikoa kadhaa ambayo ni duni katika vigezo vingi. Hii inajumuisha mikoa ya Lindi, Singida, Shinyanga, Pwani, Mara na Tabora.

Kwa ujumla, tofauti katika umaskini na vigezo vya ustawi wa jamii kati ya wanaume na wanawake ni ndogo kuliko tofauti za kijiografia. Wanawake wana kipato kidogo kuliko wanaume, ingawaje ni vigumu kupima tofauti katika matumizi kati ya mtu na mtu. Asilimia ya kaya ambazo wakuu wake wa kaya ni wanawake imeongezeka katika miaka ya 1990 ingawaje sio maskini ikilinganishwa na kaya ambazo wakuu ni wanaume. Wanawake watu wazima wana kiwango kidogo cha elimu kuliko wanaume watu wazima. Hata hivyo, viwango vya sasa vya uandikishaji watoto mashuleni ni vikubwa zaidi kwa wasichana.

Vipimo vya ustawi wa jamii vinaonyesha maendeleo kiasi katika miaka ya 1990. Uchumi umekuwa anuai na matumizi ya kaya yameongezeka. Asilimia ya watu maskini imeshuka kiasi, ingawaje idadi yao imeongezeka kutokana na ukuaji wa idadi ya watu. Hata hivyo, maendeleo haya mara kwa mara huandamana na kupanuka kwa tofauti ya kipato kati ya matabaka katika jamii. Maendeleo yametokea zaidi katika maeneo ya mjini, hasa Dar es Salaam, wakati katika maeneo ya vijijini ni madogo sana. Kaya ambazo wakuu wake wa kaya hawakusoma au hawajiwezi kiuchumi zimeshuhudia ongezeko halisi la umaskini katika kipindi hicho. Maendeleo katika muongo uliopita hayakuenea kwa usawa.

Vigezo Muhimu kutoka kwenye Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi

Kigezo	1991/92	2000/01
KAYA NA HALI YA NYUMBA		
Wastani wa ukubwa wa kaya	5.7	4.9
Wastani wa Asilimia ya watu Tegemezi	40	42
Asilimia ya Kaya zenye wakuu wa kaya wanawake	18	23
Asilimia ya Kaya zenye paa la kisasa	36	43
Asilimia ya Kaya zenye kuta za kisasa	16	25
Wastani wa idadi ya watu wanaolala katika chumba	2.6	2.4
Asilimia ya Kaya zenye umeme	9	12
Asilimia ya Kaya zinazotumia choo	93	93
Asilimia ya Kaya zinazomiliki redio	37	52
ELIMU, AFYA NA MAJI		
Asilimia ya Wanaume watu wazima wenye elimu yoyote	83	83
Asilimia ya Wanawake watu wazima wenye elimu yoyote	68	67
Asilimia ya watu wazima wanaojua kusoma na kuandika	-	71
Uwiano halisi wa uandikishaji shule (Net Enrolment Ratio) za msingi	-	59
Asilimia ya watoto wenye umri wa miaka 7-13 wanaosoma	57	61
Uwiano halisi wa uandikishaji (Net Enrolment Ratio) Sekondari (Kidato I-IV)	-	5
Asilimia ya kaya zilizo ndani ya umbali wa Km.2 mpaka Shule ya Msingi	66	63
Asilimia ya watu wote wanaomuona mtoa huduma za afya	-	69
Asilimia ya Kaya zilizo ndani ya umbali wa Km. 6 mpaka Kituo cha huduma ya afya ya msingi	75	75
Asilimia ya kaya zenye vyanzo vya maji vilivyo jengewa	46	55
Asilimia ya kaya zilizo ndani ya umbali wa Km.1 mpaka kwenye maji ya kunywa	50	55
SHUGHULI ZA KIUCHUMI		
Asilimia ya watu wazima ambao shughuli yao kuu ni kilimo	73	63
Asilimia ya watoto wenye umri wa miaka 5-14 ambao wanafanya kazi	-	62
Wastani wa eneo la ardhi inayomilikiwa na kaya za vijijini (ekari)	-	6.0
Asilimia ya kaya zenye mwanakaya mwenye akaunti benki	18	6
MATUMIZI NA UMASKINI		
Wastani wa Gharama za Matumizi kwa mtu mmoja (2000/01 Tsh., kwa siku 28)	8,686	10,120
Asilimia ya gharama ya matumizi ya chakula	71	65
Asilimia ya watu walio chini ya kiwango cha umaskini wa chakula	22	19
Asilimia ya watu walio chini ya kiwango cha mahitaji ya msingi	39	36
Kigezo cha tofauti ya kipato (Gini coefficient)	0.34	0.35
Jumla ya matumizi ya kaya maskini sana ambazo ni asilimia 20 ya kaya zote kama asilimia ya jumla ya matumizi ya kaya nchini	7	7

1. KAYA YA TANZANIA BARA

Tanzania Bara, asilimia 84 ya kaya zinamiliki nyumba wanamoishi, ingawaje katika maeneo ya mjini, zaidi ya theluthi moja zinapanga nyumba za watu binafsi.

Kaya zaidi zina wakuu wa kaya wanawake

Kumekuwepo na ongezeko kubwa katika asilimia ya kaya zinazoongozwa na wanawake – kuanzia asilimi 18 katika mwaka 1991/92 hadi asilimia 23 katika mwaka 2000/01. Maeneo ya mijini ukiondoa Dar es Salaam yana asilimia kubwa zaidi ya kaya za aina hiyo. (Kielelezo na. 1)

Hali hii imeambatana na kushuka kwa ukubwa wa kaya – kutoka wastani wa watu 5.7 hadi watu 4.9 – na ongezeko dogo la asilimia ya kaya zinazoongozwa na watu walio zaidi ya miaka 65.

Hali ya nyumba ni bora zaidi

Kumekuwepo na ongezeko katika asilimia ya kaya zinazoishi kwenye nyumba zilizojengwa kwa vifaa vya kisasa – zege, mawe, saruji na mabati. Kiasi cha asilimia 43 ya nyumba Tanzania Bara sasa zimeezekwa kwa bati na asilimia 25 zina kuta za zege, sementi, mawe au matofali ya kuokwa au kuchomwa. Maendeleo haya kwa kawaida yamekuwa makubwa zaidi katika maeneo ya mijini – lakini pia yanaonekana katika maeneo ya vijijini. (Kielelezo na. 2)

KIELELEZO NA. 1 ASILIMIA YA KAYA AMBAZO MKUU WAKE WA KAYA NI MWANAMKE, KWA ENEO



Kwa ujumla, asilimia 10 ya kaya za Watanzania Bara zimeunganishwa kwenye umeme wa gridi ya Taifa na nyongeza ya asilimia 2 ya kaya zinatumia umeme kutoka vyanzo vingine. Uunganishwaji kwenye umeme wa gridi ya taifa umeenea zaidi katika maeneo ya mjini –Asilimia 59 ya kaya za Dar es Salaam na asilimia 30 katika maeneo mengine ya mijini. Katika maeneo ya

vijijini, ni asilimia 2 tu ya kaya ndizo zilizounganishwa. Katika miaka ya 1990, uunganishaji uliongezeka katika maeneo ya mijini lakini ulionyesha mabadiliko madogo katika maeneo ya vijijini.

Dar es Salaam, Kilimanjaro na Arusha ni mikoa yenye asilimia kubwa zaidi ya kaya zilizounganishwa kwenye gridi ya Taifa. Zile za Shinyanga na Kagera zimeunganishwa kwa kiasi kidogo sana. Karibu asilimia 9 ya kaya hutumia umeme kama chanzo chao kikuu cha mwangaza wa ndani, wakati asilimia 84 hutegemea mafuta ya taa.

KIELELEZO NA. 2 ASILIMIA YA KAYA ZINAZOISHI KATIKA NYUMBA ZILIZOJENGWA KWA VIFAA VYA KISASA



Matumizi ya umeme kwa ajili ya kupikia ni ya nadra – imeripotiwa na karibu asilimia moja ya kaya. Kuni na mkaa ndio nishati muhimu inayotumika kupikia – hutumiwa na asilimia 78 na asilimia 14 ya kaya kwa mtiririko huo. Katika maeneo ya mjini, matumizi ya umeme kwa kuangaza yameongezeka, wakati matumizi yake kwa kupikia yameshuka. Yawezekana hili linaakisi kuongezeka kwa gharama zake.

Kiasi cha asilimia 93 ya kaya zinaripoti kuwa zinatumia vyoo; zaidi ya asilimia 90 katika maeneo ya vijijini. Hayajakuwepo mabadiliko kwa zaidi ya muongo mmoja sasa. Asilimia ambazo hazitumii choo zinatofautiana kimkoa, asilimia kubwa ikiwa Tanga, Arusha na Mara.

Katika miaka ya 1990, kumekuwepo na kushuka kwa wastani wa umbali wa huduma nyingi muhimu – kama vile masoko, maduka, na vituo vya usafiri. Hata hivyo, umbali kwenda mahakama ya mwanzo na vyama vya ushirika vya msingi umeongezeka. Katika maeneo ya vijijini kuna wastani mkubwa wa umbali kwenda kupata huduma muhimu, kukiwa na kaya zinazotembea wastani wa kilomita 37 kutoka benki na kilomita 18 kutoka kituo cha polisi.

Kaya za mijini zinaelekea kumiliki bidhaa za kudumu zaidi kuliko za maeneo ya vijijini. Umiliki uliongezeka katika miaka ya 1990. Wakati ongezeko lilikuwa kubwa zaidi Dar es Salaam na maeneo mengine ya mijini, vijijini nako kulionyesha ongezeko la umiliki wa bidhaa zisizotumia umeme, vikijumuisha baiskeli na redio. Kiasi cha asilimia 46 ya kaya za vijijini sasa zinamiliki redio.

Kitaifa, asilimia 84 za kaya Tanzania Bara zinamiliki nyumba wanamoishi, ingawa kwa mijini zaidi ya theluthi wanapanga. Kumekuwepo na mabadiliko madogo sana ya umiliki katika muongo.

2. ELIMU



Kiasi cha asilimia 59 ya watoto wenye umri wa miaka saba hadi kumi na tatu waliandikishwa darasa la I-VII mwaka 2000/01. Uandikishaji ni mkubwa maeneo ya mjini.

Maendeleo kidogo katika miaka 10

Robo ya Watanzania watu wazima hawana elimu na asilimia 29 hawajui kusoma wala kuandika. Kiasi cha asilimia 30 katika maeneo ya vijijini hawana elimu, ikilinganishwa na asilimia 8 tu Dar es Salaam na asilimia13 katika maeneo mengine ya mjini. Ni idadi ndogo Sana ya watu wazima maeneo ya vijijini wamesoma zaidi ya elimu ya msingi (Jedwari Na. 1)

Wanawake wana uwezekano wa karibu mara mbili ya wanaume wa kotukuwa na elimu. Hususani, Wanawake wa vijijini wana hali ngumu, zaidi ya theluthi hawana elimu kabisa na asilimia 41 hawawezi kusoma wala kuandika. (Kielelezo na. 3)

Asilimia ya watu wazima wenye angalau elimu kidogo ni kubwa zaidi Dar es Salaam, Kilimanjaro, Ruvuma, Iringa na Mbeya; na ndogo zaidi Lindi, Pwani na Shinyanga.

JEDWALI NA. 1 KIWANGO CHA JUU ZAIDI CHA ELIMU KILICHOFIKIWA NA WATU WAZIMA (%)

	Dar es Salaam		Maeneo mengine ya mjini		Vijijini		Tanzania Bara	
	91/92	00/01	91/92	00/01	91/92	00/01	91/92	00/01
Hawana elimu	9.0	7.6	13.0	13.1	28.0	29.0	24.9	25.2
Elimu ya watu wazima tu	1.2	0.9	1.3	1.1	3.7	2.3	3.3	2.1
Elimu ya msingi 1-4	8.6	6.4	14.3	9.8	15.8	12.8	15.2	11.9
Elimu ya msingi 5-8	57.0	60.6	58.8	57.6	49.0	52.5	50.7	53.8
Elimu ya Sekondari	18.8	16.6	9.9	13.6	2.2	2.4	4.2	5.0
Diploma/Chuo Kikuu	1.6	2.9	0.4	0.7	0.0	0.1	0.2	0.4
Mafunzo ya vyeti	3.8	5.1	2.3	4.2	1.2	0.8	1.5	1.6
Jumla	*100.0*	*100.0*	*100.0*	*100.0*	*100.0*	*100.0*	*100.0*	*100.0*

KIELELEZO NA. 3 ASILIMIA YA WATU WAZIMA WENYE ELIMU KWA JINSIA NA ENEO



KIELELEZO NA. 4 ASILIMIA YA WATOTO WANAOHUDHURIA SHULE, KWA UMRI NA ENEO



KIELELEZO NA.5: ASILIMIA YA WATOTO WENYE UMRI WA MIAKA 7-13 WALIOKUWA SHULENI MWAKA 1991/92 NA 2000/01



Maendeleo katika kiwango cha elimu ya watu wazima katika muongo uliopita yalikuwa kidogo. Kulikuwa na ongezeko la asilimia ya watu waliomaliza elimu ya msingi lakini hapakuwa na kushuka kwa wazi katika asilimia ya watu wazima wasio na elimu.

Kiasi cha asilimia 59 ya watoto wenye umri wa kuanzia miaka saba hadi kumi na tatu waliandikishwa darasa la I-VII mwaka 2000/01. Viwango vya uandikishaji ni vikubwa zaidi mijini kuliko vijijini – asilimia 71 ikilinganishwa na asilimia 50. Wasichana katika umri huo wameandikishwa wengi zaidi kuliko wavulana; ingawaje wanaume wanaelekea kuendelea kubaki shuleni hata wakiwa na umri mkubwa. Mikoa ya Kilimanjaro, Dar es Salaam, Iringa na Mbeya ina viwango vikubwa zaidi vya uandikishaji wa elimu ya msingi; Lindi na Shinyanga ina viwango vidogo zaidi.

Wapo watoto wengi katika shule za msingi wenye umri mkubwa - sababu mojawapo ikiwa ni kuchelewa kuanza shule, hususan vijijini (kielelezo Na. 4). Matokeo yake ni kwamba hata watoto wengi walio shuleni mara nyingi wanakuwa katika madarasa ya chini kuliko umri wao. Kwa mfano, kiasi cha asilimia 82 ya watoto wenye umri wa miaka 13 wameandikishwa darasa la V au chini ya hapo. (Jedwali Na. 2)

Kulikuwa na ongezeko dogo la watoto wenye mahudhurio endelevu katika elimu ya msingi katika muongo uliopita. Asilimia ya watoto wa miaka saba hadi kumi na tatu wanaoenda shuleni imeongezeka kutoka 57 mpaka 61. Uandikishaji uliongezeka zaidi maeneo ya mjini lakini uliongezeka kwa asilimia mbili tu katika maeneo ya vijijini. (Kielelezo Na. 5).

Uandikishaji katika elimu ya sekondari ni mdogo kuliko ule wa msingi. Asilimia 5 tu ya watoto wenye umri wa miaka 14 hadi 17 wanaandikishwa kidato cha I-IV. Uandikishaji katika umri huo ni mkubwa zaidi Dar es Salaam - asilimia 19, na mdogo zaidi katika maeneo ya vijijini, ambako asilimia 2 ya watoto hawa wako kidato cha I-IV.

JEDWALI NA. 2 MAHUDHURIO DARASANI KWA UMRI (%)

Umri	Cheke-chea	Kiwango							zaidi ya D.VII	Jumla
		I	II	III	IV	V	VI	VII		
7	37.2	52. 5	9.3	1.0						*100.0*
8	13.0	51.2	29.3	5.4	1.1					*100.0*
9	8.0	41.2	31.1	13.4	4.7	1.4				*100.0*
10	5.6	23.8	33.4	26.2	9.1	1.4	0.4			*100.0*
11	1.0	17.8	24.5	26.9	19.3	7.7	2.4	0.4		*100.0*
12	1.3	8.1	12.1	25.0	27.0	18.8	6.4	1.2	0.1	*100.0*
13	1.6	3.7	7.8	17.5	24.7	26.3	13.7	3.9	0.9	*100.0*

Umbali kwenda shule

Karibu theluthi mbili ya kaya Tanzania Bara ziko ndani ya umbali wa kilomita mbili kutoka shule ya msing; hata vijijini asilimia 58 ziko ndani ya umbali huu. Hii inaonesha kuwa umbali sio kipingamizi kikubwa cha kusoma katika shule za msingi kwa kaya nyingi. Mikoa iliyo na kaya zilizo mbali sana na shule za msingi ni Shinyanga, Kagera na Dodoma, na mikoa iliyo na shule zilizo karibu zaidi na shule za msingi ni Dar es Salaam, Kilimanjaro, Lindi, Ruvuma na Rukwa. Kaya ziko mbali zaidi na shule za Sekondari – kwa vijijini, robo ziko kilomita 20 au zaidi.

3. AFYA

Zaidi ya nusu ya wagonjwa wanaomuona mtoa huduma za afya wanatumia huduma za serikali.

Watoto na Wazee wana uwezekano mkubwa zaidi wa kuugua.

Katika maeneo ya vijijini, kiasi asilimia 28 ya watu Tanzania Bara walikuwa wagonjwa au waliumia katika muda wa majuma manne kabla ya utafiti kufanywa, ikilinganishwa na asilimia 19 Dar es Salaam na asilimia 24 katika maeneo mengine ya mjini.

KIELELEZO NA. 6 ASILIMIA YA WATU WAGONJWA AU WALIOUMIA KATIKA KIPINDI CHA WIKI NNE KABLA YA UTAFITI, KWA RIKA NA JINSIA



Watoto chini ya umri wa miaka mitano na wazee ni makundi yenye uwezekano zaidi wa kuugua au kuumia. Wanawake wanaugua mara nyingi zaidi ya wanaume. Hata hivyo miongoni mwa watoto walio chini ya miaka mitano, wavulana huugua mara kwa mara kuliko wasichana.

Kiasi cha asilimia 69 ya watu waliokuwa wagonjwa wanasema wamemwona mtoa huduma za afya. Hata vijijini, asilimia 67 wanaripoti kupata ushauri wa aina fulani. Kwa watu waliopata kuugua, ugonjwa uliotajwa mara nyingi ni homa au malaria – asilimia 69 ya watoto na asilimia 60 ya watu wazima.

Mgawanyo sawa (50/50) kati ya serikali na sekta binafsi.

Kiasi cha asilimia 54 ya waliomwona mtoa huduma za afya walitumia huduma za serikali, (Jedwali Na.3). Utumiaji wa huduma za serikali ni mdogo zaidi Dar es Salaam, ambako matumizi ya sekta binafsi ni makubwa sana. Watoa huduma binafsi wana mchango mkubwa hata vijijini, ambako huduma za waganga wa jadi na wamishenari pia hutumika sana.

JEDWALI NA.3 AINA YA SEHEMU YA USHAURI KWA WATU WALIOKWENDA KWA MHUDUMU WA AFYA YOYOTE (%)

Chanzo	Dar es Salaam	Maeneo mengine ya Mjini	Vijijini	Tanzania Bara
Serikali				
Zahanati/Hospitali	40.0	37.9	42.3	41.6
Hospitali ya Mkoa	2.9	12.2	1.7	3.1
Kituo cha Afya ya Jamii	6.6	8.3	10.9	10.4
Binafsi, cha kisasa				
Zahanati/hospitali	47.4	31.8	19.3	22.3
Daktari/wa meno	1.9	5.1	7.6	7.0
Hospitali/zahanati ya Misheni	1.2	6.6	10.1	9.2
Nyinginezo				
Mganga wa jadi	2.6	5.5	17.2	15.0
Duka la dawa	4.1	3.1	2.3	2.5
Nyinginezo	0.7	0.8	1.9	1.7

Tanbihi: Kwa kuwa ushauri unaweza kuwa umetoka katika zaidi ya chanzo kimoja. Jumla inaweza kuzidi Asilimia 100.

Kiasi cha asilimia 11 ya watu wamemwona mtoa huduma ya afya zaidi ya mmoja. Watumiaji wanaelekea zaidi kutoa taarifa za kutokuridhishwa na watoa huduma wa serikali. Kusubiri kwa muda mrefu na ukosefu wa dawa ni malalamiko ya kawaida kuhusiana na huduma za serikali. Gharama kubwa ni malalamiko ya kawaida katika hospitali za binafsi za kisasa wakati kwa waganga wa jadi matibabu ni hafifu.

Kaya nyingi ziko umbali wa kawaida na huduma za msingi za afya ya jamii. Hata vijijini, zaidi ya asilimia 90 ziko ndani ya kilomita10 kutoka ilipo zahanati au kituo cha afya.

Zaidi ya asilimia 90 ya kaya ziko ndani ya umbali wa kilomita sita kutoka ilipo zahanati au kituo cha afya kwa Dar es Salaam, Kilimanjaro na Kigoma, wakati chini ya nusu ya kaya za Dodoma ndizo ziko ndani ya umbali huo. Wastani wa umbali wa hospitali ni kilometa 21; vijijini ni kilometa 26.

4. MAJI YA KUNYWA

Kiasi cha asilimia 44 ya kaya Tanzania Bara bado zinatumia vyanzo visivyo salama vya maji ya kunywa



Asilimia 44 ya vyanzo vya maji bado si salama

Kwa ujumla, asilimia 44 ya kaya Tanzania Bara bado zinatumia vyanzo vya maji ya kunywa ambavyo si salama, vikiwemo visima na chemchemi na maji mengi ya mito na maziwa. Asilimia 39 zinatumia maji ya bomba na asilimia nyingine 16 hutumia maji salama ya visima au chemchemi (kielelezo Na.7).

Watu katika maeneo ya mjini wanapata maji ya kunywa bora zaidi kuliko watu walio vijijini. Kiasi asilimia 53 ya kaya za vijijini zinategemea maji yasiyo salama, wakati ambapo asilimia 86 ya kaya za Dar es Salaam na asilimia 76 katika maeneo mengine ya mjini zina aina fulani ya maji ya bomba. Kaya za vijijini pia zinalazimika kutembea mwendo mrefu kupata maji, ni asilimia 49 tu ya kaya zilizo ndani ya kilometa moja. Hii inalinganishwa na asilimia 85 na asilimia 73 ya kaya za Dar es Salaam na maeneo mengine ya mjini,(Jedwali Na. 4).

Watu wa mjini na vijijini wameona mwenendo tofauti katika usambazaji wa maji ya kunywa katika miaka ya 1990. Katika maeneo ya vijijini vyanzo vilikuwa bora zaidi, asilimia ya kaya zinazotegemea vyanzo visivyo salama ikipungua kutoka asilimia 64 hadi 53. Katika maeneo ya mijini, tofauti na vijijini, kumekuwa na kushuka kwa asilimia ya kaya zenye maji ya bomba katika makazi.

KIELELEZO NA. 7 VYANZO VYA MAJI YA KUNYWA (%)



Kuna tofauti kubwa katika vyanzo vya maji ya kunywa kati ya mkoa na mkoa. Robo tatu au zaidi ya kaya katika mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Kigoma na Mbeya zina vyanzo salama, wakati ambapo robo tatu ya kaya katika mikoa ya Lindi na Tabora zinategemea maji yasiyo salama.

JEDWALI NA. 4 : VYANZO VYA MAJI YA KUNYWA KWA ENEO (%)

	Dar es Salaam		Maeneo mengine ya mjini		Maeneo ya Vijijini		Tanzania Bara	
	91/92	00/01	91/92	00/01	91/92	00/01	91/92	00/01
Maji ya Bomba	**93.0**	**85.7**	**72.7**	**75.6**	**24.5**	**28.3**	**35.9**	**39.3**
Mabomba binafsi nyumbani	22.1	13.7	20.3	15.1	1.1	0.8	5.2	3.8
Mabomba mahali pengine	71	72.1	52.4	60.5	23.5	27.5	30.7	35.5
Vyanzo vingine salama	**3.8**	**7.9**	**10.9**	**12.4**	**10.3**	**17.6**	**10.0**	**16.2**
Visima vya umma (salama)	3.5	4.7	10.5	7.5	9.4	13.3	9.2	11.8
Visima binafsi (salama)	0.4	3.2	0.4	4.2	0.7	1.4	0.7	2.0
Chemchemi (salama)	0.0	0.0	0.0	0.7	0.2	2.9	0.2	2.4
Vyanzo visivyo salama	**1.8**	**3.6**	**10.1**	**11.2**	**63.9**	**53.2**	**52.1**	**43.6**
Visima vya umma (visivyo salama)	1.7	2.2	5.5	5.1	26.5	21.2	21.9	17.5
Visima binafsi (visivyo salama)	0.1	1.0	0.8	1.2	2.6	3.8	2.2	3.2
Chemchemi (zisizo salama)	0.0	0.2	0.4	2.0	11.6	12.4	9.2	10.0
Mto, bwawa au ziwa	0.0	0.1	3.4	3.0	23.2	15.8	18.8	12.8
Vyanzo vingine	**1.4**	**2.8**	**6.2**	**0.8**	**1.2**	**0.9**	**2.0**	**1.0**
Jumla	*100.0*	*100.0*	*100.0*	*100.0*	*100.0*	*100.0*	*100.0*	*100.0*

Ni kiasi cha theluthi moja tu ya kaya katika mikoa ya Mara na Shinyanga zimo ndani ya kilometa moja kutoka chanzo cha maji ya kunywa, lakini zaidi ya asilimia 80 zimo ndani ya umbali huo katika Mikoa ya Ruvuma na Dar es Salaam.

5. SHUGHULI ZA UCHUMI

Wanawake wameonekana kwa kiasi kikubwa kuachana na kilimo - kama shughuli kuu kutoka asilimia 77 mwaka 1991/92 mpaka asilimi 63 mwaka 2000/01

Wengi bado wanategemea kilimo

Ingawa Watanzania walio wengi bado wanategemea kilimo, kaya zina aina nyingi za shughuli za kiuchumi (kielelezo Na.8). Kiasi cha asilimia 70 sasa zina mkuu wa kaya anayefanya shughuli za kilimo au uvuvi ikilinganishwa na asilimia 75 kwa mwaka 1991/92. Upungufu mkubwa zaidi wa umuhimu wa kilimo unaonekana katika shughuli za watu wazima wote katika kaya – ukiwa umeshuka kama shughuli kuu kutoka asilimia 73 hadi asilimia 63, (jedwari Na. 5).

KIELELEZO NA. 8 SHUGHULI KUU ZA WATU WAZIMA (%)



Pia kumekuwepo na kushuka kwa ajira serikalini na katika mashirika ya umma – kutoka asilimia 5.2 ya watu wazima hadi asilimia 2.5. Kushuka huku ni kukubwa zaidi Dar es Salaam, ambako ajira imeshuka kutoka asilimia 21 ya watu wazima hadi asilimia 7. Kuna ongezeko la ajira katika sekta binafsi na katika kujiajiri, ambazo sasa ni shughuli kuu za asilimia 40 ya watu wazima Dar es Salaam na asilimia 31 katika maeneo mengine ya mjini

Wanawake wamepunguza kwa kiasi kikubwa zaidi shughuli za kilimo – toka kuwa shughuli kuu ya asilimia 77 ya wanawake mwaka 1991/92 hadi asilimia 63 mwaka 2000/01. Wanaume wamekabiliwa na kushuka kidogo, lakini wameathirika zaidi na kuhama kutoka ajira serikalini na mashirika ya umma kwenda katika sekta binafsi. Kiasi cha asilimia 42 ya kaya zinaripoti kuwa na shughuli ya biashara – asilimia kubwa zaidi iko mijini, hasa miji mingine mbali na Dar es Salaam.

Katika mikoa mingi, kiasi cha asilimia 60 hadi 80 ya watu wazima wanaripoti kuwa kilimo ndiyo shughuli yao kuu. Kiwango ni kidogo kwa mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Mbeya tu ambako kuajiriwa na kujiajiri ni kitu cha kawaida kuliko sehemu nyingine.

JEDWALI NA. 5 SHUGHULI ZA UCHUMI ZA WATU WAZIMA, KWA ENEO (%)

	Dar es Salaam		Maeneo mengine ya mjini		Maeneo ya Vijijini		Tanzania Bara	
	91/92	00/01	91/92	00/01	91/92	00/01	91/92	00/01
Ukulima, ufugaji au uvuvi	2.3	3.0	43.0	26.9	83.4	75.8	72.8	63.2
Mwajiriwa – Serikalini	8.7	3.8	9.1	5.1	2.1	1.2	3.4	1.9
Mwajiriwa – mashirika ya umma	12.7	3.1	3.2	1.6	0.6	0.2	1.8	0.6
Mwajiriwa –Sehemu nyingine	9.7	16.0	4.1	9.6	1.0	1.9	2.0	4.1
Kujiajiri na kuajiri watu wengine	17.3	5.9	13.3	4.5	2.0	1.0	4.5	1.9
Kujiajiri bila kuajiri watu wengine	1.1	18.1	0.5	16.7	0.2	2.9	0.3	6.1
Msaidizi katika shughuli za familia asiyelipwa	4.8	10.5	4.7	13.0	1.1	7.5	1.8	8.5
Mama wa nyumbani, mtunza nyumba au kazi ndogondogo katika kaya	21.6	19.2	10.1	11.2	1.0	4.0	3.6	6.2
Mwanafunzi	14.7	8.6	6.4	4.3	5.7	2.0	6.3	2.8
Asiye na shughuli	7.2	11.6	5.4	7.2	2.9	3.5	3.5	4.6
Jumla	*100.0*	*100.0*	*100.0*	*100.0*	*100.0*	*100.0*	*100.0*	*100.0*

Karibu asilimia 89 ya kaya za vijijini zinaripoti kumiliki ardhi kwa ajili ya kilimo au kwa ajili ya malisho, kiwango sawa na mwaka 1991/92. Kiwango cha kilimo cha utumiaji mashine miongoni mwa kaya za vijijini ni kidogo – ambapo asilimia 11 wanamiliki plau, na karibu asilimia 0.2 tu wanamiliki trekta.

Ni asilimia 6 tu ya kaya zina mwanakaya mmoja au zaidi wenye akaunti ya benki na asilimia 4 tu wanashiriki katika vikundi visivyo rasmi vya kuweka akiba. Matumizi ya benki na vikundi vingine vya kuweka akiba yamepungua katika miaka ya 90.

Shughuli za watoto

Kiasi cha asilimia 62 ya watoto wenye umri wa miaka mitano hadi kumi na nne wanafanya aina mojawapo ya kazi; zaidi kidogo ya nusu ya watoto hao wanafanya kazi na kusoma (Jedwali Na. 6). Wasichana wanaelekea kufanya kazi zaidi kuliko wavulana – asilimia 64 ya wasichana ikilinganishwa na asilimia 59 ya wavulana.

JEDWALI NA. 6 SHUGHULI ZA WATOTO KATIKA SIKU SABA KABLA YA UTAFITI, KWA RIKA NA JINSIA (%)

Shughuli	Miaka 5-9	Miaka 10-14	Jumla 5-14
Kilimo, uvuvi au ajira na hawasomi	8.6	11.3	9.9
Kazi za ndani au biashara za familia na hawasomi	25.9	10.3	18.2
Kilimo, uvuvi au ajira na kusoma	1.1	5.9	3.5
Kazi za ndani au biashara za familia na kusoma	16.1	44.7	30.1
Kusoma tu	16.7	22.4	19.5
Hawafanyi lolote	31.6	5.4	18.8
Jumla	*100.0*	*100.0*	*100.0*

6. MATUMIZI YA KAYA

Baada ya kutilia maanani mfumuko wa bei, wastani wa matumizi ya kaya umepanda kwa asilimia 17 kati ya mwaka 1991/92 na 2000/01

Dalili za kuinuka/kupanda kipato cha kaya

Wastani wa matumizi ya kila mtu ni mkubwa Dar es Salaam – mara 2.6 zaidi ya wastani wa vijijini wa kiasi cha shilingi za Tanzania 8,500 kwa mwezi.

KIELELEZO NA. 9 MGAO WA MATUMIZI YA CHAKULA NA VIFAA (%)



Baada ya kutilia maanani mfumuko wa bei, matumizi ya kaya yamepanda kwa karibu asilimia17 kati ya mwaka 1991/92 na mwaka 2000/01, ikiashiria kuongezeka kwa pato la kaya. Dar es Salaam imeonyesha kupanda kwa kiasi kikubwa zaidi – karibu asilimia 47. Maeneo ya vijijini yameshuhudia ongezeko la karibu asilimia 11 tu. Matokeo yake, tofauti kati ya maeneo ya mjini na vijijini iliongezeka, (Jedwali Na. 7).

Chakula kinachukua asilimia 65 ya jumla ya matumizi ya kaya, (kielelezo Na.9). Kaya za vijijini zinatumia asilimia kubwa zaidi katika chakula; zile za Dar es Salaam zinatumia kiasi kidogo zaidi. Asilimia ya matumizi kwa chakula ilishuka katika miaka ya 1990 kutoka asilimia 71 mpaka asilima 65, sambamba na mwenwedo wa kukua kwa kipato halisi. Matumizi ya chakula yalipungua kwa asilimia 14 Dar es Salaam na asilimia 5 maeneo ya vijijini.

JEDWALI NA. 7 MWENENDO WA MATUMIZI HALISI YA MTU MMOJA (KWA SIKU 28 MWAKA 2000/01 TSH).

	Dar es Salaam	Maeneo mengine ya mjini	Maeneo ya vijijini	Tanzania Bara
2000/01	21,949	14,377	8,538	10,120
1991/92	14,896	12,733	7,661	8,686
% Ongezeko	47	13	11	17

Kaya sasa zinanunua zaidi chakula, na zinalima kidogo zaidi chakula kinacholiwa katika kaya kuliko ilivyokuwa mwaka 1991/92.

JEDWALI LA 8 ASILIMIA YA MGAO WA AINA YA MATUMIZI

	Dar es Salaam		Maeneo mengine ya mjini		Maeneo ya vijijini		Tanzania Bara	
	91/92	00/01	91/92	00/01	91/92	00/01	91/92	00/01
Chakula-kilichonunuliwa	67.1	52.2	56.9	52.8	30.5	35.2	35.8	38.6
Chakula-kilichozalishwa na kaya	0.7	2.1	9.4	7.9	41.8	31.8	35.5	26.8
Bidhaa za kudumu	7.6	7.8	7.4	8.0	7.2	7.1	7.2	7.3
Matumizi ya matibabu	0.9	2.9	1.2	2.4	0.9	2.1	0.9	2.2
matumizi ya elimu	1.1	4.0	1.1	3.0	0.8	1.6	0.8	2.0
Bidhaa zingine zisizokuwa za kudumu	22.6	31.1	24.0	25.9	18.9	22.1	19.7	23.1
Jumla (%)	*100.0*	*100.0*	*100.0*	*100.0*	*100.0*	*100.0*	*100.0*	*100.0*
Kwa matumizi ya chakula	*67.8*	*54.2*	*66.3*	*60.7*	*72.3*	*67.0*	*71.3*	*65.4*

Mgawo wa matumizi ya kaya katika elimu na matibabu umeongezeka kwa zaidi ya mara mbili. Hivi sasa vyote vina kiasi cha asilimia 2 ya wastani wa matumizi ya kaya, kulinganisha na chini ya asilimia 1 mwaka 1991/92. Kaya za Dar es Salaam zinatumia asilimia kubwa katika afya na elimu – kwa pamoja zinafanya kiasi cha asilimia 7 za jumla ya matumizi yao – wakati ambapo kaya za vijijini zinatumia chini ya asilimia 4.

UPIMAJI

Matumizi yalikusanywa kwa muda wa mwezi mmoja

Utafiti ulikusanya kumbukumbu ya kila kitu kilichotumiwa na kaya iliyohojiwa katika kipindi cha mwezi mmoja.

Ilijumuisha chakula na vifaa vingine vilivyonunuliwa; ilijumuisha pia chakula ambacho kililimwa na kaya na kutumiwa katika mwezi huo.

Utafiti haukujumuisha matumizi ambayo siyo ya kawaida, kwa mfano ununuzi wa pembejeo kwa ajili ya mashamba yaliyolimwa na kaya.

7. UMASKINI WA KIPATO NA MATABAKA.

Kiwango cha umaskini kinahusiana sana na elimu ya mkuu wa kaya. Kiasi cha asilimia 51 ya watu ni maskini kama mkuu wa kaya hana elimu

Umaskini bado ni changamoto – hasa maeneo ya vijijini

Kumekuwa na kushuka kidogo umaskini wa kipato kwa kiasi cha asilimia tatu katika muongo uliopita. Kiasi cha asilimia 36 ya watu Tanzania Bara sasa wako chini ya kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi na asilimia 19 wapo chini ya kiwango cha umaskini wa chakula ikilinganisha na asilimia 39 na asilimia 22 mwaka 1991/92 (Jedwali Na. 9). Kushuka huku si kukubwa kiasi cha kuwa muhimu kitakwimu.

KIELELEZO NA.10 ASILIMIA YA IDADI YA WATU WALIO CHINI YA KIWANGO CHA UMASKINI WA MAHITAJI YA MSINGI



Maeneo ya vijijini yana kiwango kikubwa cha umasikini, yakiwa na asilimia 39 ya idadi ya watu walio chini ya kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi ikilinganishwa na asilimia 18 Dar es Salaam na asilimia 26 katika maeneo mengine ya mjini. Katika muongo uliopita, umaskini umeshuka zaidi Dar es Salaam (Kielelezo Na.10).

Idadi ya watu wanaoishi katika umaskini iliongezeka katika miaka ya 90 kwa sababu ya ongezeko la watu. Kwa kutumia makisio ya taifa ya idadi ya watu, sasa kuna watu milioni 11.4 Tanzania Bara walio katika kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi ikilinganishwa na watu milioni 9.5 katika mwaka 1991/92 (Jedwali Na. 10).

Umaskini unaendelea kuwa mzigo vijijini – asilimia 87 ya watu maskini wanaishi vijijini. Kuongezeka kwa matumizi ya kaya kulienda pamoja na ongezeko dogo katika tofauti ya mapato kati ya matabaka. Kipimo cha tofauti ya mapato katika jamii (Gini cofficient) kilioongezeka kutoka 0.34 hadi 0.35. Watu wenye kipato cha juu - asilimia 20 ya idadi ya watu wanatumia jumla ya asilimia 44 ya matumizi ya kaya nchini, ikilinganishwa na asilimia 43 mwaka 1991/92; wale masikini zaidi - asilimia 20 wanatumia asilimia 7 tu ya matumizi nchini katika miaka yote miwili. Ongezeko kubwa la tofauti ya matabaka lilikuwa katika maeneo ya mjini, hasa Dar es Salaam.

JEDWALI NA. 9 ASILIMIA YA IDADI YA WATU WALIO KATIKA UMASKINI

	Dar es Salaam		Maeneo mengine ya mjini		Vijijini		Tanzania Bara	
	91/92	00/01	91/92	00/01	91/92	00/01	91/92	00/01
Umaskini wa chakula	13.6	7.5	15.0	13.2	23.1	20.4	21.6	18.7
Umasikini wa Mahitaji ya msingi	28.1	17.6	28.7	25.8	40.8	38.7	38.6	35.7

JEDWALI NA.10 IDADI YA MASIKINI KWA MAENEO (KIWANGO CHA UMASIKINI WA MAHITAJI YA MSINGI)

	Dar es Salaam		Maeneo mengine ya mjini		Vijijini		Tanzania Bara	
	91/92	00/01	91/92	00/01	91/92	00/01	91/92	00/01
Idadi ya masikini ('000)	369	325	888	1,136	8,223	9,926	9,481	11,388
Asilimia ya masikini	3.9	2.9	9.4	10.0	86.7	87.2	100.0	100.0

Ulinganishaji wa kiwango cha umaskini wa kipato kimkoa hauna budi kufanywa kwa uangalifu. Hata hivyo, mikoa minne inajitokeza mara zote kuwa na umaskini chini ya wastani: Lindi, Mara, Singida na Shinyanga. Dar es Salaam na Mbeya ina viwango vidogo vya umasikini kuliko wastani.

UPIMAJI

Jinsi kiwango cha umasikini (poverty line) kinavyoainishwa

Kiwango cha umaskini wa chakula ni matumizi ya chini ya mtu mmoja yatakayompatia kalori 2,200 kila siku kwa mwezi mmoja, kwa kuzingatia chakula kinachotumiwa na asilimia 50 ya idadi ya watu maskini. Kiwango cha juu kidogo cha umaskini wa "mahitaji ya msingi" kinaruhusu matumizi mengine ya kawaida kama nguo.

Kiwango cha umaskini wa chakula kilikuwa Tsh. 5,295 mwaka 2000/01-ikilinganishwa na Tsh. 2,083 mwaka 1991/92. Viwango vya umaskini wa mahitaji ya msingi vilikuwa Tsh. 7,253 (2000/01) na Tsh. 2,777 (1991/92).

Kiwango cha umaskini kitaifa ni lazima kirekebishwe kufuatana na bei zinazotumika na kaya katika maeneo mbalimbali. Kwa mfano, bei za vyakula vingi Dar es Salaam ni kubwa kuliko maeneo ya vijijini, kwa hiyo, inagharimu zaidi kununua chakula cha kutosha kupata kalori 2,200 kwa Dar es Salaam. Kwa sababu hiyo, viwango vya umaskini viko juu zaidi kwa kaya zinazoishi huko.

Kwa mfano, mwaka 2000/01 kiwango cha umaskini wa chakula kilikuwa Tsh. 6,719 Dar es Salaam wakati katika maeneo ya vijijini kilikuwa Tsh. 5,107.

Wenye elimu ndogo na wakulim ni miongoni mwa maskini sana

Viwango vya umaskini vina uhusiano mkubwa na elimu ya mkuu wa kaya. Kiasi cha asilimia 51 ya watu ni maskini kama mkuu wa kaya hana elimu ikilinganishwa na asilimia 12 ikiwa mkuu wa kaya ana elimu zaidi ya kiwango cha elimu ya msingi (kielelezo Na.11).

KIELELEZO NA.11 ASILIMIA YA WATU MASIKINI, KWA ELIMU YA MKUU WA KAYA



Kaya ambazo zinategemea kilimo, kwa kiasi fulani zina kiwango cha juu kidogo cha umaskini kuliko wastani, hasa zile zinazotegemea uuzaji wa mifugo.

Katika miaka ya 1990 umaskini ulipungua zaidi miongoni mwa waajiriwa na waliojiajiri, hasa waajiriwa katika sekta binafsi. Tofauti na hivyo, umaskini uliongezeka katika kaya zenye mkuu wa kaya ambaye hakujishughulisha kiuchumi au hakuwa na elimu na katika kaya zenye idadi kubwa ya wategemezi.

Maskini wanafaidika kidogo zaidi na huduma za jamii

Kiasi cha asilimia 50 ya watoto wenye miaka saba hadi kumi na nne kutoka kwenye kaya maskini zaidi walikuwa wanasoma ikilinganisha na asilimia 66 kutoka katika kaya zenye unafuu. Asilimia ya watoto kutoka katika kaya maskini zaidi wanaosoma imepungua katika miaka ya 1990. Hii inahatarisha kuwepo kwa mzunguko wa umaskini, kwa vile utafiti pia umeaonyesha kuwa mapato ya watu wazima yanahusiana sana na elimu yao.

Maskini hawaripoti viwango vya juu vya kuugua na kuumia kama kaya zenye kipato cha juu. Wanapougua, kwa kiasi fulani wana uwezekano mdogo wa kumuona mtoa huduma za afya, pamoja na mtoa huduma wa afya wa serikali, kuliko watu wanaotoka kutoka katika kaya nyingine.

Kiasi cha asilimia 54 ya kaya maskini sana zinategemea vyanzo vya maji ya kunywa visivyo salama ikilinganishwa na asilimia 40 ya kaya nyingine. Wastani wa umbali mpaka kwenye chanzo cha maji ya kunywa pia ni mkubwa kwa kaya maskini sana.

8. KIPATO KILICHORIPOTIWA

Kuajiriwa na ajira binafsi zinachangia kiasi cha asilimi 71 ya pato la kaya Dar es Salaam na asilimia 57 katika maeneo ya vijijini

Vyanzo mbalimbali

Mauzo ya mazao ya kilimo yalikuwa chanzo kikuu cha pato la fedha kwa asilimia 62 ya kaya ikilinganishwa na asilimia 67 mwaka 1991/92. Mazao ya chakula yamebakia kuwa chanzo pekee muhimu – chanzo kikuu cha asilimia 41 ya kaya, sawa na mwaka 1991/92. Umuhimu wa mazao ya biashara umeshuka. Sasa ni chanzo kikuu cha fedha kwa asilimia 17 tu ya kaya.

Kilimo huchangia kiasi zaidi kidogo ya nusu ya kipato chote cha kaya (kielelezo Na. 12). Pamoja na umuhimu wa jumla wa kilimo katika maeneo ya vijijini, kiasi cha asilimia 40 ya kipato chote cha kaya vijijini kinatokana na vyanzo vilivyo nje ya uzalishaji mashambani (Jedwari Na. 11).

JEDWALI LA 11 MGAWO WA JUMLA YA KIPATO CHA KAYA KWA KUZINGATIA CHANZO (%)

Chanzo	Dar es Salaam	Maeneo mengine ya Mjini	Vijijini	Tanzania Bara
Ajira	41.7	24.5	8.3	12.5
Kujiajiri (ukiondoa kilimo)	29.1	32.8	17.8	20.6
Kipato kutokana na kilimo	1.9	19.6	60.4	51.4
Kodi, riba, magawio	2.0	1.3	0.3	0.6
Uhawilishaji	12.1	10.1	7.1	7.8
Mapato mengine	13.2	11.7	6.0	7.2
Jumla	*100.0*	*100.0*	*100.0*	*100.0*

KIELELEZO CHA 12 MGAWO WA JUMLA YA KIPATO CHA KAYA KWA KUZINGATIA CHANZO CHA MAPATO (%)



Kuajiriwa na kujiajiri vinachangia kiasi cha asilimia 71 ya pato Dar es Salaam. Katika maeneo mengine ya mjini vyanzo hivyo vinachangia asilimia 57 ya pato na vyanzo vya kilimo vinatoa asilimia 20 nyingine.

Kaya za vijijini zinategemea mapato kutoka vyanzo vingi zaidi kuliko kaya za mjini; asilimia 65 zinaripoti vyanzo zaidi ya vitatu. Vyanzo hivyo mbalimbali vinaonekana kuwa ni njia muhimu kwa kaya za vijijini kukuza kipato chao, kwa kuwa kaya zenye idadi kubwa ya vyanzo zina kipato kikubwa.

Kipato kinatofautiana kwa jinsia na elimu

Watu wenye elimu inayozidi sekondari wana pato mara nne zaidi ya pato la wenye elimu ndogo. Tofauti hizi ni kubwa hasa Dar es Salaam, ambapo wenye elimu kubwa walio wengi wanapata kipato mara kumi zaidi ya walio na elimu ya chini.

KIELELEZO CHA 13 WASTANI WA PATO LA MWEZI KWA MTU MMOJA, KWA JINSIA NA KIWANGO CHA ELIMU (TSH '000) (BAR CHART)



Pia kuna tofauti kubwa kati ya wastani wa vipato vya wanaume na wanawake. Wanaume wanapata pato karibu mara mbili ya pato la wanawake. Mambo mengi yanachangia katika tofauti hizi lakini yanaendelea kuwepo hata wakati ambapo tunatilia maanani tofauti ya viwango vya elimu kijinsia (kielelezo Na.13)

	DODOMA	ARUSHA	KILIMANJARO	TANGA	MOROGORO	PWANI	DAR ES SALAAM	LINDI	MTWARA	RUVUMA	IRINGA	MBEYA	SINGIDA	TABORA	RUKWA	KIGOMA	SHINYANGA	KAGERA	MWANZA	MARA	TANZANIA BARA
KAYA NA HALI YA NYUMBA																					
% Kaya zenye wakuu wa kaya wanawake	27	21	26	24	20	18	21	20	20	14	31	29	29	23	15	11	21	23	22	29	23
% Kaya zilizo na nyumba zenye kuta za kisasa	23	18	39	6	28	6	88	4	11	67	28	32	7	6	32	39	6	13	10	23	25
% Kaya zilizo na nyumba zenye paa la kisasa	33	53	85	41	45	33	98	16	28	42	48	53	21	24	16	21	24	53	42	43	44
% kaya zilizounganishwa na umeme wa gridi ya taifa	6	11	18	7	10	6	59	5	5	5	6	9	5	4	4	6	3	2	5	10	10
% Kaya zinazotumia choo	92	84	97	81	94	98	94	98	93	99	99	96	90	97	88	99	90	95	92	86	93
Wastani wa umbali kutoka sehemu wanapopatia kuni (Kaya za vijijini, Km)	2.7	2.8	1.5	3.2	2.8	1.7	n/a	1.6	3.2	2.0	3.6	1.9	10.4	2.5	5.0	6.2	4.2	1.9	1.9	2.9	3.1
Wastani wa umbali wa duka la karibu (Kaya za vijijini, Km)	1.8	2.8	0.2	1.8	2.3	1.0	n/a	1.1	0.6	0.8	0.9	3.9	1.6	2.1	2.6	1.6	2.7	2.1	1.3	1.6	1.8
ELIMU																					
% ya watu wazima wote wasio na elimu	31	20	12	31	26	39	8	44	28	15	16	16	27	31	30	28	40	25	27	24	25
% ya wanaume watu wazima wasio na Elimu	22	15	7	23	16	24	5	34	19	9	9	9	18	23	19	21	29	13	20	12	17
% ya wanawake watu wazima wasio na elimu	38	24	15	38	35	52	11	52	36	20	24	23	35	39	40	33	49	35	33	34	32
Kiwango halisi cha uandikishaji elimu ya msingi	58	53	81	50	61	56	71	44	59	63	76	69	61	55	61	48	46	59	52	62	59
Wastani wa umbali wa shule ya msingi (Km)	2.8	1.9	0.9	2.3	1.7	1.7	0.8	1.2	1.1	0.9	1.5	1.3	1.9	3.0	1.3	1.7	2.7	2.5	1.7	1.8	1.8
Wastani wa umbali wa shule ya sekondari (Km)	19.4	6.4	5.0	18.8	16.0	13.1	2.5	25.1	16.6	9.2	12.7	8.7	9.5	15.0	21.3	14.3	20.5	12.0	9.4	6.9	12.6
AFYA																					
% Wastani wa idadi ya waliougua katika wiki nne kabla ya utafiti	34	23	23	23	32	34	19	20	28	22	25	24	29	27	24	21	32	34	30	29	27
% Wastani wa idadi ya waliougua katika wiki nne kabla ya utafiti ambao walimuona mtoa huduma ya afya	69	62	74	87	70	83	80	61	63	76	79	61	65	69	47	69	68	64	65	72	69
Walimuona mtoa huduma ya afya wa serikali (%)	58	48	40	64	55	69	49	68	71	52	46	47	45	79	59	67	41	59	48	46	54
% Kaya zilizo ndani ya km 6 toka zahanati/kituo cha afya	49	73	95	62	75	74	98	67	87	85	63	90	82	58	82	93	65	74	75	71	75
Wastani wa umbali kutoka hospitali (Km)	35.3	11.8	9.5	29.0	24.0	24.5	2.8	22.7	19.2	21.0	18.9	20.7	12.8	13.7	66.0	20.2	18.9	25.1	30.1	13.4	21.3
MAJI YA KUNYWA																					
% ya kaya zinazotumia maji ya bomba au vyanzo salama vya maji	65	58	77	46	70	35	94	19	52	53	54	75	61	25	55	76	39	32	53	40	55
% ya kaya zilizo ndani ya umbali wa Km 1 kutoka chanzo cha maji ya kunywa (wakati wa kiangazi)	49	49	58	41	61	56	84	47	41	90	72	75	51	54	63	55	33	45	40	31	55
SHUGHULI ZA KIUCHUMI																					
% ya kaya zinazotegemea kilimo	67	42	56	67	63	62	3	72	69	77	67	55	60	69	76	76	68	81	71	70	62
% ya watoto (5-14) wanaofanya kazi	67	73	64	80	55	57	28	40	46	73	60	53	52	39	51	60	69	68	84	55	62
Wastani wa ukubwa wa eneo linalomilikiwa na kaya ya kijijini (ktk ekari)	6.0	3.4	1.5	3.9	4.3	2.9	n/a	2.7	3.2	6.2	2.9	3.7	4.5	6.8	8.6	3.7	14.1	4.0	6.8	8.0	5.3
MATUMIZI NA UMASKINI																					
Wastani wa matumizi ya mtu ('000' shs. Za Tz) kwa siku 28	8.5	10.3	11.2	9.3	10.0	10.5	21.9	9.5	12.4	9.6	11.2	12.6	6.9	10.4	6.7	7.3	8.0	9.0	8.1	8.0	10.1
% ya watu walio chini ya kiwango cha umasikini wa chakula	13	25	11	11	14	27	7	33	17	27	10	8	28	9	12	21	22	18	30	36	19
% ya watu wailo chini ya kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi	34	39	31	36	29	46	18	53	38	41	29	21	55	26	31	38	42	29	48	46	36
% ya matumizi kwa chakula	67	69	69	70	68	69	54	74	66	60	65	61	69	68	58	65	67	63	64	66	65

MIKOA YA TANZANIA BARA

Shukrani

Ripoti hii inawakilisha matokeo ya juhudi za watu wengi. Wafanyakazi wengi wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu wameshiriki katika Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya wa mwaka 2000/2001. Ulisimamiwa na Said Aboud. Emilian Karugendo, Mlemba Abassy na Ephygenia Woisso walikuwa maofisa wasaidizi. Uingizaji wa takwimu na usahihishaji wa makosa ulisimamiwa na David Danda, Joshua Mwaisemba, Fred Matola na Joy Sawe. Uchambuzi wa takwimu umefanywa na Mlemba Abassy, David Danda na Fred Matola.

Shukrani ziende kwa Oxford Policy Management (UK) na washirika wake, ambao walitusaidia kuandaa sampuli, mchanganuo wa takwimu, uchambuzi na kuandika ripoti. Shukrani pekee ziende kwa Patrick Ward, Trudy Owens (Centre for the Study of African Economies), Ahmed Makbel, Jeff Mwaijonga na Goodchance Aminiel Mariki (Data Vision International), Juan Munoz, Victor Canales, Ludovic Carraro, Donato Speroni na Sofia Barletta wa Odysseus, Neil Chalmers, George Clark, Mohamed Rashid Lugongo na Zakayo Msokwa wa Chuo cha Takwimu cha Afrika ya Mashariki na David Nyange (ESRF).

Pia napenda kuwashukuru wajumbe wa Vikundi vya Kiufundi vya Mfumo wa Ufuatiliaji Umaskini Tanzania (PRSP Technical Working Groups), ambao maoni na ushauri wao umeimarisha uchanganuzi. Nao ni Arthur Mwakapugi (Ofisi ya Raisi - Mipango na Ubinafsishaji), Profesa Joseph Semboja (REPOA), Dk. Servacius Likwelile (Ofisi ya Makamu wa Rais), Profesa H.K.R. Amani (ESRF), Alice Nkhoma-Wamunza (UDSM), Prof. Marjorie Mbilinyi (UDSM), Valerie Leach (UNICEF), Arthur Van Diesen (UNDP), Prof. Benno Ndulu (Benki ya Dunia), Alana Albee (UK DFID), Tomoko Enoki (JICA) na Jackson Biswaro (JICA).

Utafiti ulisaidiwa na wabia wetu wa maendeleo. Ningependa kuishukuru Idara ya Maendeleo ya Kimataifa UK (UK DFID-Tanzania), ambayo pamoja na kutoa fedha kwa ajili ya utafiti pia imegharimia katika uchambuzi wake na kusaidia katika kukabiliana na changamoto wakati wote wa zoezi hilo. Fedha pia zilitolewa na serikali za Sweden (SIDA), Canada (CIDA), Netherlands (Ubalozi wa Netherlands), Denmark (DANIDA), Japan (JICA), Marekani (USAID), Norway na UNDP. Benki Kuu ya Tanzania ilisaidia katika hatua ya kuhamasisha michango na pia ilisaidia kutoa fedha.

Mwisho, ningependa kutoa shukrani kwa kaya zote na wadadisi ambao walishiriki katika kukusanya takwimu hizi nchi nzima.

Cletus P.B.Mkai
Mkurugenzi Mkuu
Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Ripoti hii inaonesha (inatoa) vidokezo vya
Utafiti wa mapato na matumizi ya kaya
binafsi 2000/01,
uliofanywa na
Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).
Utafiti huu ulihusisha kaya zaidi ya 22,000 kutoka
mikoa yote ishirini Tanzania bara.

Matokeo ya utafiti huu ni msingi wa kupima maendeleo
ya sera za Serikali katika kupunguza umaskini. Hali
kadhalika yanaonesha mwenendo wa vigezo vya
umaskini katika miaka ya 90.

Ripoti hii ni chanzo muhimu
cha taarifa kwa yeyote anayefuatilia
masuala ya umaskini Tanzania.